


# القرآن الحكيم

## QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by

Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy  
(Former Chief Kadhi of  
Zanzibar & Kenya)



Ina Aya 30

SURATUL MULK

Ina Makara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Ametukuka yule ambaye Mkononi mwake umo ufalme (wote); Naye ni mwenye uweza juu ya kila kitu.

تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمَلَكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝

2. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Msamaha;

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ۝

3. Ambaye ameumba mbingu saba zilizo tabakatabaka, (moja juu ya moja); huoni tafauti yoyote katika uumbaji wa Mwingi wa rehema. Hebu rudisha macho (yako uzidi kutazama); je unaona kosa?

الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا مَّا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِن تَفْوُتٍ ۚ قَارِعِمْ الْبَصَرَ ۚ هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٍ ۝

4. Tena rudisha macho (yako) mara nyingi zaidi; jicho lako litarudia hali ya kuwa limehizika na umechoka.

ثُمَّ ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنقَلِبْ إِلَيْكَ الْبَصَرُ خَاسِئًا وَهُوَ حَسِيرٌ ۝

5. Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu hii kwa mataa, na Tumeyafanya ili kuwapigia mashetani; na Tumewaweka tayari adhabu ya Moto uwakao (kwa nguvu).

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحٍ وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيَاطِينِ وَأَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابَ السَّعِيرِ ۝

6. Na kwa waliomkufuru Mola wao iko adhabu ya Jahanamu (inawangojea). Na ni marejeo mabaya yaliyoje!

وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَدْرِبُهُمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ ۖ وَيَسَّسُ الْأَعْيُنُ ۝

7. Watakapotupwa humo watasikia rindimo (mngurumo) lake, na hali ya kuwa inafoka

إِذَا الْقَوَارِيحُ سُمِعُوا لَهَا شَهيقًا وَهِيَ تَفُورٌ ۝

8. Unakaribia kupasuka kwa hasira (yake juu ya wabaya). Kila mara litakapotupwa humo kundi (la wabaya) walinzi wake watawauliza: "Je! Hakukufikieni Mwonyaji?"

تَكَادُ تَمَيَّزُ مِنَ الْقُبْحِ ۚ كَلَّمَا نَتَقَىٰ فِيهَا فُجُورٌ سَأَلْتَهُم خِزْنُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ۝

الْقُبْحُ الْقُبْحُ الْقُبْحُ الْقُبْحُ

1. Sura hii Mtume alikuwa anapenda kila mtu awe anayaweka machoni madhumuni ya Aya zake, kama alivyoitaja Hadithi hii Imam Attabarany na Imam Abd bin Humeid na wengineo. Na Mtume alikuwa ana dasturi ya kuisoma kila usiku kabla ya kulala, kama alivyotaja Imam Attirmdhy na wengineo. Yote ni makumbusho ya uweza na neema za Mungu.

Anaona mtu humu kuwa mambo yote yamo katika mkono wa Mwenyezi Mungu, kwa hivyo amuabudu Yeye amuombe Yeye na amtegemee Yeye tu basi.

Mambo yote ni ya Mungu  
Ndiye Pweke mwenye quwa

Atakalo ndilo huwa  
Mwenye amri na shani.

9. Watasema: "Kwa nini? Alitujia Muonyaji, lakini tulikadhibisha na tulisema: 'Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote, nyinyi hamumo ila katika upotofu (upotevu) mkubwa?'"

10. Na watasema: "Kama tungalikuwa tunasikia au tungalikuwa na akili hatungekuwa katika watu wa Motoni (leo)."

11. Wakakiri dhambi zao; (lakini hapana faida). Basi kuangamia kumewastahikia watu wa Motoni.

12. Hakika wale wanaomuogopa Mola wao, na hali ya kuwa hawamuoni, watapata msamaha na malipo makubwa.

13. Na ficheni kauli zenu au zidhihirisheni; hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani, (seuze yanayosemwa au kufanywa).

14. Oh! Asijue aliyumba! Naye ndiye avijuaye visivyojulikana na vinavyojulikana.

15. Yeye ndiye aliyefanya ardhi iwe inaweza kutumika (kwa kila myatakayo) kwa ajili yenu. Basi nendeni katika pande zake zote na kuleni katika riziki zake, na kwake Yeye ndiyo marejeo (yenu nyote).

16. Je! Mnadhani muko salama kwa (Mwenyezi Mungu) ambaye uko mbinguni (ufalme wake mkubwa) ya kuwa Yeye hatakuudidimizeni ardhini, tahamaki hiyo inataharaki (na nyinyi, inakudidimizeni chini kama walivyodidimizwa hao wa zamani)?

17. Au mnadhani mko salama kwa (Mwenyezi Mungu) ambaye yuko mbinguni (ufalme wake mkubwa), ya kuwa Yeye hatakuleteni kimbunga chenye changarawe (zikuangamizeni changarawe hizo)? Mtajua vipi maonyo yangu.

18. Na bila shaka walikadhibisha wale wa kabla yao; basi kulikuwaje kukasirika kwangu? (Niliwaangamiza kabisa. Na wao wataangamizwa vile vile).

19. Je! hawawaoni ndege walioko juu yao namna wanavyozinyosha (mbawa zao) na kuzikunja? Hakuna anayewazuilia (wasianguke) ila (Mwenyezi

قَالُوا يَا قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ هَذَا فَكَدَّبْنَا وَكُنَّا  
مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِنْ شَيْءٍ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا فِي

صَلَلٍ كَبِيرٍ ⑩

وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي

أَصْحَابِ السَّعِيرِ ⑪

فَاعْتَرَفُوا بِذَنبِهِمْ هَ فَسَحَقًا لِأَصْحَابِ السَّعِيرِ ⑫

إِنَّ الَّذِينَ يُحْشَوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ

وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ⑬

وَاسْرَأُوا قَوْلَكُمْ أَوَاجْهًا بِهِنَّ إِنَّهُنَّ عَلَيْكُمْ بَدَائِلُ

الضُّمُورِ ⑭

غَا. أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ⑮

هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ ذُلُولًا فَأَمْشُوا فِي

مَنَازِلِهَا وَكُلُوا مِنْ رِزْقِهِ وَأَلْيَسَ النَّشُورُ ⑯

أَمْ أَنْتُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ أَنْ يَخِفَّ بِكُمْ الْأَرْضُ

فَإِذَا هِيَ تَمُورٌ ⑰

أَمْ أَنْتُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ أَنْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ

حَاصِبًا، فَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرٍ ⑱

وَلَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَكَيْفَ كَانَ

نَكِيرٍ ⑲

أَوَلَمْ يَرَوْا إِلَى الطَّيْرِ فَوْقَهُمْ صَافٍ وَيَقْبِضْنَ ⑳

قَعْدَاتٍ يُخَذَّلْنَ

12. Huku ndiko kucha Mungu, sio kujionyesha mbele za watu — akiwa faragha hakuna shetani kumshinda yeye. Aya hii ina tafsiri mbili. Moja ndiyo hiyo tuliyoitaja juu. Na nyingine ni hii tuliyoitilia haya maelezo. Tafsiri yake inakuwa: "Hakika wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu wanapokuwa faragha, watapata msamaha na malipo makubwa."

15. Aya hii ni moja ya Aya zinazohimiza watu wawache nchi zao kama hawatengenekewi hapo; wende nchi nyingine. Na ziko nyingi kama hizi, kama Aya ya 97 ya Suratun Nisaa.

Mungu) Mwingi wa rehema. Hakika Yeye anaona kila kitu.

20. Au ni lipi hilo jeshi lenu liwezalo kukunusuruni pasipo (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema? Hawako makafiri ila katika kudanganyika.

21. Au ni nani ambaye atakupeni riziki kama Akizuia riziki zake (Mwenyezi Mungu)? Bali wao wanaendelea tu katika uasi na chuki.

22. Je! Anayekwenda akisinukia kwa uso wake ni muongofu au anayekwenda sawasawa katika njia iliyonyoka?

23. Sema: “Yeye ndiye aliyekuumbeni na akakupeni mashikio na macho na nyoyo.” Ni kidogo kabisa shukurani yenu.

24. Sema: “Yeye ndiye aliyekutawanyeni katika ardhi, na kwake mtakusanywa.”

25. Na wao wanasema (kwa kejeli): “Lini (itatimizwa) ahadi hii (ya kuja Kiama) ikiwa mnasema kweli?”

26. Sema: “Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu; na hakika mimi ni Muonyaji (tu) abainishaye (aliyotumwa kuyabainisha).”

27. Lakini watakapokiona karibu, nyuso za waliokufuru zitahuzunika (kweli kweli siku hiyo), na itasemwa: “Hayo ndiyo mliyokuwa mkiyaomba (yaje — basi yamekuja).”

28. Sema: “Niambieni kama Mwenyezi Mungu akiniangamiza mimi na walio pamoja nami au akiturehemu, basi ni nani atakayewalinda makafiri na adhabu iumizayo?”

29. Sema: “Yeye ndiye Mwingi wa rehema; tunamuamini Yeye, na tunamtegemea Yeye; na karibuni hivi mtajua ni nani aliye katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri.”

30. Sema: “Mwaonaje, kama maji yenu yakiwa yamezama, (yamedidimia chini), basi nani atakuleteeni maji (safi) yatiririkayo?” (Ni Yeye tu Mwenyezi Mungu; basi muabuduni Yeye tu).

مَا يُدْعُونَ إِلَّا الرَّحْمَنَ ۚ إِنَّهُ يُكَلِّمُ سَمْعِي ۚ بَصِيرًا ۝١٨

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ جُنْدُكُمْ يَنْصُرُكُمْ مِّنْ دُونِ  
الرَّحْمَنِ ۚ إِنَّ الْكُفْرَ لَإِنَّا فِي عُرُوشٍ ۝١٩

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي يَرْزُقُكُمْ إِنْ أَمْسَكَ رِزْقَهُ ۚ بَلْ  
لَجُّوا فِي عُتُوٍّ وَ نُفُورٍ ۝٢٠

أَفَمَن يَتَّبِعِي مُكِبًّا عَلَىٰ وَجْهِهِ أَهْدَىٰ  
أَمَّن يَتَّبِعِي سَوِيًّا عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ۝٢١

قُلْ هُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ  
وَ الْآبْصَارَ ۚ وَ الْآفَاقَةَ ۚ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ۝٢٢

قُلْ هُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ ۚ وَإِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ۝٢٣  
وَ يَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝٢٤


قُلْ إِنَّا الْعِلْمُ عِنْدَ اللَّهِ ۚ وَإِنَّا أَنَا نَذِيرٌ  
مُّبِينٌ ۝٢٥

فَلَمَّا رَأَوْهُ زُلْفَةً سَيِّئَاتُ الَّذِينَ كَفَرُوا  
وَ قِيلَ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُدَّعُونَ ۝٢٦

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَهْلَكَنِيَ اللَّهُ ۚ وَمَنْ مَّعِيَ أَوْ  
رَحِمَنَا ۚ فَمَنْ يُجِيرُ الْكَافِرِينَ ۚ مِّنْ عَذَابِ الْإِلْمِ ۝٢٧

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ أَمَّنَّا بِهِ ۚ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا ۚ  
فَتَعَلَّمُونَ مَن هُوَ فِي صَلَاتِ مُّبِينٍ ۝٢٨

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَصْبَحَ مَاؤُكُمْ غَوْرًا ۚ فَمَن  
يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مُّبِينٍ ۝٢٩



Ina Aya 52

SURATUL QALAM

Ina Makaru 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

1. Nuun. (Naapa kwa) kalamu na yale wayaandikayo (kwa kalamu hizo)

ن وَالْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُونَ ﴿١﴾

2. Kwa neema ya Mola wako wewe si mwendawazimu. (Makafiri wakimwambia Mtume — kwa ajili ya kumtukana tu — kuwa yeye ni mwendawazimu).

مَا أَنْتَ بِنِعْمَةِ رَبِّكَ بِمَجْمُوعٍ ﴿٢﴾

3. Na kwa hakika una malipo yasiyokatika (yataendelea maisha).

وَإِنَّ لَكَ لَأَجْرًا غَيْرَ مَمْنُونٍ ﴿٣﴾

4. Na bila shaka una tabia njema kabisa.

وَ إِنَّكَ لَعَلَىٰ خَلْقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

5. Basi karibuni hivi utaona, na wao pia wataona

فَتَسْبُحُوا وَيُحْمَدُونَ ﴿٥﴾

6. Ni nani mwenye wazimu miongoni mwenu; (ni wewe au wao. Wao ndio wendawazimu).

بِأَيْتِكُمُ الْمُفْتُونُ ﴿٦﴾

7. Hakika Mola wako anamjua aliyepote katika njia yake na anawajua sana walioongoka.

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِسَبِّ مَن صَلَّىٰ عَنْ سَبِيلِهِ

وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٧﴾

8. Basi usiwatii wanaokadhibisha.

فَلَا تُطِعِ الْمُكَذِّبِينَ ﴿٨﴾

9. Wanapenda ungalikuwa laini (kwao; ukawapaka mafuta kwa nyuma ya chupa), nao wakawa laini (kwako; wakakupaka mafuta kwa nyuma ya chupa).

وَذُوًّا لَوْ تَدْرَهُنَّ فَيُدْهِمُونَ ﴿٩﴾

10. Wala usimtii kila muapaji sana, aliye dhalili

وَلَا تُطِعْ كُلَّ حَلَّافٍ مَّهِينٍ ﴿١٠﴾

11. Msengenyaji (msemaji watu), aendaye akitia fitina

هَمَّازٍ مَّشَاءٍ بِمِيمٍ ﴿١١﴾

12. Azuiaye kheri, anayedhulumu viumbe wenziwe, anayemuasi Mwenyezi Mungu

مَثَاءٍ لِلْخَيْرِ مُعْتَدٍ أَن يُنْفِثَهُ ﴿١٢﴾

13. Mwenye roho ngumu; (na) juu ya hayo (hana nafuu hata chembe), kama kitu kilichopachikwa kisipachikike vizuri.

عُتْلٍ بَعْدَ ذٰلِكَ رَبِّهِمْ ﴿١٣﴾

2-7. Anasifiwa Mtume na analiwazwa na anakanushiwa wazimu waliokuwa wanamsambikizia (wanamsingizia) makafiri. Akutukanaye hakuchagulii tusi.

8-15. Zinatajwa baadhi ya sifa za watu wabaya ambazo inataka mtu ajiepushe nazo. Na inaambiwa mtu asikubali kufanya unafiki katika dini, akabania haki. Eleza haki tu, kila mtu aisikiye.

14. Kwa ajili ya kuwa ni mwenye mali na watoto (ndio anatakabari?).

أَنْ كَانَ ذَا مَالٍ وَبَنِينَ ۝

15. Anaposomewa Aya zetu anasema: “(Hizi) ni simulizi za uwongo za watu wa zamani.”

إِذَا نُفِخَ فِيهِنَّ أَصْوَابُنا وَأَنَا فَوَازِينَ ۝

16. Tutamtia kovu juu ya pua yake, (tutamdhalilisha).

سَنَسِفُهُ عَلَى الْخُرُطُومِ ۝

17. Hakika tutawatia mtihanini (Makureshi) kama tulivyowatia mtihanini wenye shamba, walipoapa kwamba watayavuna (mazao yake) itakapokuwa asubuhi (ili wasionekane na maskini wakaombwa)

إِنَّا بَلَوْنَهُمْ كَمَا بَلَوْنَا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ إِذْ أَقَامُوا كَيْصِرُهَا مُصِيبِينَ ۝

18. Wala hawakumvua (maskini hata mmoja, hawakusema: “Ila Fulani na Fulani na . . . ndio tutawapa.”)

وَلَا يَسْتَنْتُونُ ۝

19. Basi ulilifikia (shamba hilo) msiba mkubwa utokao kwa Mola wako; na hali wao walikuwa wamelala

فَطَافَ عَلَيْهَا طَافٍ مِنْ رَبِّكَ وَهُمْ نَائِمُونَ ۝

20. Ikawa kama lililoungua

فَأَصْبَحَتْ كَالصَّرِيمِ ۝

21. Asubuhi wakaitana

فَتَنَادَوْا مُصِيبِينَ ۝

22. Ya kwamba: “Nendeni mapema kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna (bila kuonekana na maskini).”

أَنْ أَعْدُوا عَلَى حَرْثِكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝

23. Basi walikwenda na huku wakinong'onezana

فَانطَلَقُوا وَهُمْ يَتَخَفَتُونَ ۝

24. Ya kuwa: “Leo maskini asiingie humo mwenu ”

أَنْ لَا يَدَّخُلَهَا يَوْمَ عَلَيْكُمْ مَسْكِينٌ ۝

25. Na wakenda asubuhi, hali wanadhani kuwa wanao uweza wa kuzuia (maskini).

وَعَدُوا عَلَى حَرْدٍ قَدِيرِينَ ۝

26. Basi walipoliona (limeungua vile walidhani kuwa silo) wakasema: “Bila shaka tumepotea, (Siko huku; silo shamba letu hili; tumepotea)”

فَلَمَّا رَأَوْهَا تَلَوَّا إِنَّا لَصَالِتُونَ ۝

27. (Walipotazama zaidi wakayakinisha kuwa ndilo walisema). — “Bali tumenyimwa (mavuno yake).”

بَلَّ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ۝

28. M-bora wao akasema: “Je! Sikukuambieni (msitie nia mbaya ya kuwazuilia haki yao maskini? Sasa) rejeeni kwa Mola wenu, mtubie kwake.”

قَالَ أَوْسَطُهُمْ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ لَوْلَا تُسَبِّحُونَ ۝

29. Wakasema: “Utukufu ni wa Mola wetu! Hakika tulikuwa madhalimu. (Basi tusamehe Mola wetu).”

قَالُوا سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ۝

30. Basi wakakabiliana kulaumiana.

فَأْتَبَلَّ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ لِيُتْلَا وَمُؤْتٌ ۝

31. Wakasema: "Hasara yetu! Hakika tulikuwa tumeruka mipaka (ya Mwenyezi Mungu)."

قَالُوا يَوْمَئِذٍ نَتَذَكَّرُ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ رَافِقِينَ ۝

32. "Asaa Mola wetu atatubadilishia (shamba) lililo bora kuliko hili; hakika sisi tunajipendeleza (sasa) kwa Mola wetu."

عَلَىٰ رَبِّنَا أَنْ يَتَّخِذَ مِنَّا مِثَالًا ۝  
رَبِّنَا مَرْغُوبُونَ ۝

33. Namna hivi inakuwa adhabu (ya Mola wako duniani). Na adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi, laiti wanalijua!

كَذَلِكَ الْعَذَابُ وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَكْبَرُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ۝

34. Hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu watakuwa na Pepo (Mabustani) yenye neema, kwa Mola wao.

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَدَّتِ الرِّيحُ الرِّيحُ ۝

35. Je! Tuwafanye wanaotii sawa na wasi?

أَفَتَجْعَلُ الْمُسْلِمِينَ كَالْمُجْرِمِينَ ۝

36. Mumekuwaje! Mnahukumu namna gani?

مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ۝

37. Au mnacho kitabu mnachokisoma (ambacho ndani yake mumeambiwa)

أَمْ لَكُمْ كِتَابٌ فِيهِ تَدْرُسُونَ ۝

38. Kuwa mtapata (siku) hiyo mnayotaka?

إِنَّ لَكُمْ فِيهِ لَمَا تَخَيَّرُونَ ۝

39. Au, mnazo ahadi juu yetu za kudumu mpaka siku ya Kiama ya kuwa mtapata mnayojihukumia?

أَمْ لَكُمْ آيَاتُنَا بِآلِقَةٍ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۝ إِنَّ

40. Waulize: "Ni nani miongoni mwao dhamini wa haya?"

لَكُمْ لَمَا تَحْكُمُونَ ۝

41. Au wana washirika (katika haya wanayoyasema)? Basi nawawalete washirika wao hao wakiwa wanasema kweli.

سَأَلَهُمْ أَيُّهُمْ بِذَلِكَ زَعِيمٌ ۝

أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ فَمَاذَا تُشْرِكُونَ ۝ إِنَّ كَانُوا

صَادِقِينَ ۝

42. (Na wawalete) hiyo siku kutakayokuwa na mateso makali, na wataitwa kusujudu lakini hawataweza

يَوْمَ يَكْشَفُ عَنْ سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ

فَلَا يَسْتَطِيعُونَ ۝

43. Macho yao yatainama chini; unyonge utawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa kusujudu walipokuwa salama (na walikataa).

خَاشِعَةً أَبْصَارُهُمْ تَرْهُقُهُمْ ذُلُّهُمْ وَقَدْ كَانُوا

يَدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ وَهُمْ سَالِمُونَ ۝

44. Niche na wanaokadhibisha Hadithi hii (Qurani). Tutawavuta kidogo kidogo katika adhabu yetu) kwa mahali wasipopajua

فَأَنزَلْنَا وَمَنْ يُكَذِّبْ بِهَذَا الْحَدِيثِ

سَنَسْتَدْرِجُهُمْ مِنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ۝

45. Na ninawapa muda; kwa hakika nguvu zangu ni kubwa (mipango yangu imara).

وَ أَمَلْنَا لَهُمْ أَنْ كِيدُوا مِنَّا وَرَأَيْنَا

46. Au unawaomba ujira; na wao wanaelemewa na gharama hiyo?

أَمْ تَسْأَلُهُمْ أَجْرًا فَهُمْ مِنْ مَغْرَمٍ مُثْقَلُونَ ۝

47. Au iko kwao (ilimu ya) siri (waliyopewa Mitume) wanaiandika; (kwa hivyo hawahitaji hii unayowaambia wewe)?

أَمْ عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ۝

35-43. Wanasutwa wanaoona kuwa hata wabaya watalipwa mema.

48. Basi subiri kwa hukumu ya Mola wako, wala usiwe kama mmezwa na Chewa (Nabii Yunusi). (Kumbuka) alipolingana, (alipomwita Mwenyezi Mungu), na hali ya kuwa amezongwa (barabara).

49. Kama isingelimfikia neema kutoka kwa Mola wake, bila shaka angalitupwa ufukoni, na hali ya kuwa mwenye kulaumiwa.

50. Lakini Mola wake alimchagua na akamfanya miongoni mwa watu wema.

51. Na wale makafiri hukurubia kukutelezesha kwa (ukodozi wa) macho yao, wanaposikia mauidha (yako); na husema: "Hakika yeye ni mwendawazimu."

52. Na hayakuwa haya, (hii Qurani) ila ni ukumbusho kwa walimwengu.

فَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُنْ كَصَاحِبِ الْحُوتِ إِذْ نَادَىٰ وَهُوَ مَكْظُومٌ ۝

أُولَٰئِكَ تَنْدَرِكُهُ رِغْمَةٌ مِّنْ رَبِّهِمْ لِيُبْذَلَ بِالْعُرَىٰ وَهُوَ تَمُومٌ ۝


فَاجْتَبَاهُ رَبُّهُ فَجَعَلَهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ۝

وَأَنَّ يَكْفُرُوا الَّذِينَ كَفَرُوا لِيَرْثُكَ بِأَبْصَارِهِمْ لَمَّا سَمِعُوا الذِّكْرَ وَيَقُولُونَ إِنَّهُ لَمَجْنُونٌ ۝

وَمَا هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعَالَمِينَ ۝

48. Tumekitaja kisa chake Nabii Yunusi mahala pengi. Pamoja ni katika Aya ya 87 ya *Suratul Anbiyau* na Aya ya 139 ya *Surat Wassaaffat*.

51. Uchukivu wa makafiri ulivyokuwa mkubwa sana juu ya Mtume hata ilikuwa hukurubia kuanguka kwa macho yao wanayomkodolea anapowapitia.



Inu Ava 52

SURATUL HAQQA

Inu Mukara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Tukio (tokeo) la haki!
2. Nini hilo Tukio, (Tokeo) la haki?
3. Na nini kitakujulisha — nini hilo tukio, (tokeo) la haki? (Kiama hicho).
4. Thamudi na Adi walikadhibisha Kiama.
5. Basi Thamudi waliangamizwa kwa balaa kubwa.
6. Na ama Adi waliangamizwa kwa upepo mkali usiozuilika
7. Aliowapelekea masiku saba na michana minane, moja kwa moja bila kusita; utaona watu wameanguka (kifudifudi) kama kwamba ni magogo ya mitende (yaliyolala chini), matupu (yawazi ndani).
8. Basi je! unamuona mmoja wao aliyebaki?
9. Na Firauni na waliomtangulia na (watu wa) miji iliyopinduliwa (chini juu), walikosa nao.
10. Wakawaasi Mitume wa Mola wao; ndipo akawakamata kwa mkamoto wenye nguvu sana.
11. Maji yalipofurika (katika zama za Nuhu) sisi tulikupandisheni katika hicho kinachokwenda (baharini, jahazi).
12. Ili tuifanye ukumbusho kwenu; na shikio lisikialo lisikie, (lidhibiti).
13. Na litakapopulizwa baragumu mpulizo mmoja tu (wakafa viumbe vyote)
14. Na ardhi na milima ikaondolewa na ikavunjwa mvunjo mmoja
15. Siku hiyo hilo tukio litakuwa limekwishatokea; (nayo ndio Kiama)

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْحَاقَّةُ ۝

مَا الْحَاقَّةُ ۝

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْحَاقَّةُ ۝

كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِطَغْوَاهُ إِذِ انبَعَثَ أَشْقَى ۝

فَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَأْذَنُوا فَحَرَمْنَا الْفَيْءَ فَأَنزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَصْبَحُوا بِطَافٍ عَلَيْهِمْ ۝

وَأَمَّا عَادُ فَاهْتَكَمُوا بِرِجِّمْ ۝

صَحَّحْنَا عَلَيْهِمُ سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَنِيَةَ أَيَّامٍ حُسُومًا فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعْجَازُ نَحْلِ خَاوِيَةٍ ۝

فَهَلْ تَرَى لَهُم مِّنْ بَاقِيَةٍ ۝

وَجَاءَ فِرْعَوْنُ وَمَنْ قَبْلَهُ وَالْمُؤْتَفِكَاتُ بِالْغَاطِقَةِ ۝

فَعَصَوْا رَسُولَ رَبِّهِمْ فَأَخَذَهُمْ أَخَذَةً رَّابِيَةً ۝

إِنَّا لَنَّا طَعْنَا الْمَاءَ فَجَاءَكُمْ فِي الْجَارِيَةِ ۝

لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَتَعِيهَا أَدُنٌ وَأَعْيِيهُ ۝

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ نَفْخَةٌ وَاحِدَةٌ ۝

وَكُحْلِمَتِ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً

وَاحِدَةً ۝

فِيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ۝

16. Na mbingu zitapasuka; basi siku hiyo, zitakuwa dhaifu kabisa

17. Na Malaika watakuwa kandoni mwake (hizo mbingu): na Malaika wa namna nane watachukua Kiti cha Enzi cha Mola wako juu yao (hawa wa dasturi).

18. Siku hiyo mtahudhurishwa — haitafichika siri yenu yoyote.

19. Basi ama yule atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kuume (kulia) atasema (kwa furaha): “Haya! Someni daftari langu (nililopewa sasa hivi).”

20. “Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu (kwa vizuri, kwani nikifanya mazuri).”

21. Basi yeye atakuwa katika maisha ya raha

22. Katika Pepo tukufu.

23. Vishada vya matunda yake vitakuwa karibu; (vinachumika bila ya taabu).

24. (Waambiwe): “Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya vitendo mlivyofanya kaitika siku zilizopita.”

25. Walakini atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kushoto basi yeye atasema: “Oo! Laiti nisingalipewa daftari langu:”

26. “Wala nisingalijua ni nini hisabu yangu:”

27. “Laiti (mauti) yangemaliza (kila kitu changu).”

28. “Mali yangu haikunifaa.”

29. “Usultani (ukubwa) wangu umenipoteta.”

30. (Kusemwe): “Mkamateni na mtieni makongwa.”

31. “Kisha mtupeni Motoni ”

32. “Tena katika mnyororo wenye urefu wa dhira sabini muingizeni, (mtatizeni).”

33. Hakika yeye alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.

34. Wala (hajihimizi wala) hahimizi (wenziwe) kulisha maskini.

35. Basi leo hapa hana rafiki mpenzi

وَأَنشَقَّتِ السَّمَاءُ فَهِيَ يَوْمَئِذٍ وَاهِيَةٌ ﴿٦٦﴾

وَأَمَّا لَكَ عَلَى أَرْجَائِكُمْ وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمَنِيَةٌ ﴿٦٧﴾

يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَى مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ﴿٦٨﴾

فَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَيَقُولُ هَذَا مَا أقرءُوا وَكَتَيْبَةٌ ﴿٦٩﴾

إِنِّي ظَنَنْتُ أَنِّي مُلْكٌ حَسَابِيَةٌ ﴿٧٠﴾

فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٧١﴾

فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿٧٢﴾

تَطُوفُهَا دَارِيَةٌ ﴿٧٣﴾

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَمْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْأَخْلَافِ ﴿٧٤﴾

وَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ ه فَيَقُولُ يُلَيِّتُنِي لِمَ أُوْتِيَ كِتَابِيَةٌ ﴿٧٥﴾

وَلَمْ أَدْر مَا حَسَابِيَةٌ ﴿٧٦﴾

يُلَيِّتُهَا كَانَتْ الْقَاضِيَةَ ﴿٧٧﴾

مَا أَعْنَى عَنِّي مَالِيَةٌ ﴿٧٨﴾

هَلْكَ عَنِّي سُلْطَنِيَةٌ ﴿٧٩﴾

حُدُودُهُ فَغَلَاؤُهُ ﴿٨٠﴾

ثُمَّ اجْعَلِيْمَ صَلَوةً ﴿٨١﴾

ثُمَّ فِي سُلْسَلَةٍ دَرَعَهَا سَبْعُونَ ذِرَاعًا فَاسْأَلُوهَا ﴿٨٢﴾

إِنَّهُ كَانَ لَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ ﴿٨٣﴾

وَلَا يَعْصِي عَلَىٰ طَعَامِ الْبِسْكَينِ ﴿٨٤﴾

فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هُنَا حَمِيمٌ ﴿٨٥﴾

36. Wala hana chakula ila maji ya usaha (wa walio Motoni)

37. Hawakili (chakula) hicho isipokuwa wakosa.

38. Basi naapa kwa mnavyoviona.

39. Na msivyoviona

40. Kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe (wa Mwenyezi Mungu) mwenye hishima (kubwa).

41. Wala si kauli ya mtunga mashairi (kama mnavyosema). Ni machache sana mnavoyaamini

42. Wala si kauli ya mchawi (kama mnavyodai). Ni kidogo kabisa kuwaidhika kwenu.

43. Ni uteremsho utokao kwa Mola wa viumbe vyote.

44. Na kama (Mtume) angelizua juu yetu baadhi ya maneno tu

45. Bila shaka tungalimshika kwa mkono wa kuume, (wa kulia)

46. Kisha kwa hakika tungalimkata mshipa mkubwa wa moyo (tukamtoa roho yake).

47. Na hapana yo yote katika nyie angeweza kutuzuia naye.

48. Kwa hakika hii (Qurani) ni mawaidha kwa wanaomcha Mungu.

49. Na kwa yakini tunajua kuwa miongoni mwenu wamo wanaokadhibisha.

50. Na itakuwa ni sikitiko, (majuto) juu ya wanaokanusha.

51. Na hakika hii ni haki ya yakini.

52. Basi litukuze jina la Mola wako aliye Mkuu.

وَلَا طَعَامٌ إِلَّا مِنْ غَسِيلٍ ۝

لَا يَأْكُلُهُ إِلَّا الْغَاطُونَ ۝

فَلَا أُقِيمُ بِمَا تُبْصِرُونَ ۝

وَمَا لَا تُبْصِرُونَ ۝

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ۝

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا تَأْتُونَ ۝

وَلَا يَقُولُ كَافٍ، قَلِيلًا مَّا تَدَّكُرُونَ ۝

تَنْزِيلٌ مِنَ رَبِّ الْعَالَمِينَ ۝

لَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ۝

لَاخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ۝

ثُمَّ لَنَقَطَعَنَّ مِنْهُ الْوَتِينَ ۝

فَمَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ۝

وَإِنَّهُ لَتَذِكْرٌ لِّلَّذِينَ ۝

وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنْكُمْ مُكَذِّبِينَ ۝

وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ ۝

وَإِنَّهُ لَحَقُّ الْيَقِينِ ۝

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ۝

44-47. Mwenyezi Mungu hana mchezo na mtu anayetaka kuyachezea maneno yake.

45. Makadiyani Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ya 46 wametia ukafiri wao tena wa kumdaia Utume mtu wao, na wakajidai kuwa An Nasfy na Ibnul Qayyim wamesema kuwa mtu akidai Utume akaishi miaka 23 baada ya madai hayo atakuwa Mtume wa kweli. Waongo kabisa; hawakusema haya hawa wala mwanachuoni mwingine yoyote wa Kiislamu. Huu ni usingizio tu wanaowasingizia hao wanavyuoni. Hao walikuwa wakitaja umri alioishi Miurme baada ya kupata Utume; wao wakapindua hivi. Mwisho wa kutaja kwetu ukafiri wa kudai Utume baada ya Nabii Muhammad ni katika marejezo ya Aya ya 40 ya *Suratul Ahzaab*.



Ina Aya 44

## SURATUL MA'ARIJ

Ina Makara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea

2. Juu ya makafiri — ambayo hapana awezaye kuizuia

3. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye utukufu mkubwa.

4. Malaika na Roho hupanda kwake katika siku ambayo muda wake ni miaka elfu hamsini. (Siku moja hiyo ya kuhisabiwa huko Kiama; kwa vishindo vyake wataiona kama miaka khamsini elfu).

5. Basi subiri kwa subira njema.

6. Kwa hakika wao wanakiona kiko mbali (hicho Kiama)

7. Nasi tunakiona kiko karibu.

8. Siku mbingu zitakapokuwa kama shaba iliyoyayuka

9. Na milima itakuwa kama sufi (inayoruka)

10. Wala jamaa hatamuuliza jamaa (yake).

11. (Ingawa) watafanywa waonane. Mwenye kosa atatamani ajikomboe katika adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa watoto wake

12. Na mke wake na ndugu yake

13. Na jamaa zake waliomzunguka kwa kila upande

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ۝

لِلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُ دَافِعٌ ۝

مِّنَ اللَّهِ ذَٰلِكَ الْمَعَارِجُ ۝

تَعْرُبُ الْمَلَكُوتُ وَالرُّوْحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ  
مُقَدَّارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ۝

فَاصْبِرْ صَبْرًا جَمِيلًا ۝

إِنَّهُمْ يَرَوْنَهُ بَعِيدًا ۝

وَوَنَرَهُ قَرِيبًا ۝

يَوْمَ تَكُونُ السَّمَاءُ كَالْمُهْلِ ۝

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ ۝

وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ۝

يُبْصِرُونَ نَهُمَ، يَوْمَ الْمَجْرُمِ كَوْفِيَتَدَىٰ مِّنْ

عَذَابٍ يَعْمِدُ بَيْنِيهِ ۝

وَصَاحِبَتِهِ وَآخِيهِ ۝

وَفَصِيلَتِهِ الَّتِي تُؤَيِّدُ ۝

11. Atamani mtu siku hiyo ajikomboe kwa kila kinachomkinika naye; lakini wapi; hakikubaliwi kikomboleo chochote kile kiwacho, hata ulimwengu mzima akiutoa.

N.B.—Na hapa husomwa *Yawmiidhin si Yawmaidhin*. Na ile ya mbele yake katika Aya ya 10 husomwa *Wala Yas-alu si Walaayus-alu*.

14. Na (kuvitoa) vyote vilivyomo katika ardhi, kisha aokoke

15. Lakini wapi! Kwa hakika huo ni Moto uwakao (barabara)

16. Unaobabua mara moja ngozi ya mwili.

17. Utamwita kila aliyegeuza mgongo na akageuka (kuyatupa mafunzo ya Qurani)

18. Na akakusanya (mali), kisha akayahifadhi (bila ya kuyatolea Zaka wala sadaka).

19. Kwa hakika Binadamu ameumbwa, hali ya kuwa mwenye papatiko

20. Inapomgusa shari huwa mwenye fazaa

21. Na inapomgusa kheri huwa anaizuilia

22. Ila wanaosali; (hao hawana sifa mbaya hiyo)

23. Ambao wanadumisha Sala zao

24. Na ambao katika mali zao iko sehemu maalumu

25. Kwa ajili ya aombaye na anayejizuilia kuomba (japo muhitaji)

26. Na ambao wanasadiki siku ya Malipo

27. Na ambao wanaiogopa adhabu (itokayo) kwa Mola wao.

28. Hakika adhabu ya Mola wao si ya kusalimika nayo mtu (mbaya).

29. Na ambao wanahifadhi tupu zao

30. Isipokuwa kwa wake zao au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi

31. Lakini wanaotaka kinyume cha haya, basi hao ndio wanaoruka mipaka.

32. Na ambao wanaangalia amana zao na ahadi zao (maagano yao)

33. Na ambao ni imara katika ushahidi wao

34. Na ambao wanazihifadhi Sala zao (hawazipuuzi).

وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ يُنْحِيهِ ۝

كَلَّا إِنَّهَا لَأَنْظٌ ۝

نَزَّاعَةً لِّلشُّونِ ۝

تَدْعُوا مَنَ أَدْبَرَ وَتَوَلَّى ۝

وَجَمَعَ فَأَوْعَى ۝

إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ۝

إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ۝

وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ۝

إِلَّا الْمَصَلِينَ ۝

الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ۝

وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ۝

لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ۝

وَالَّذِينَ يُصَدِّقُونَ بَيِّوَاتِ الدِّينِ ۝

وَالَّذِينَ هُمْ مِّنْ عَذَابِ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ ۝

إِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ مَا مُنِنَ ۝

وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ۝

إِلا عَلَىٰ أَرْوَاحِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ

فَأَنزَلُومُ غَيْرُ مَلُومِينَ ۝

فَمَن ابْتَغَىٰ وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعُدُونَ ۝

وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ۝

وَالَّذِينَ هُمْ بِشَهَادَتِهِمْ قَائِمُونَ ۝

وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ۝

19-35. Linatajwa umbile baya la binadamu ambalo akifanya mema haya yaliyotajwa litamwondokea Umbile hilo baya, awe aliyefuzu duniani na Akhera.

35. Hao ndio watakaokuwa katika Mabustani wakihishimiwa.

أُولَئِكَ فِي جَنَّاتٍ مُّكْرَمُونَ ﴿٣٥﴾

36. Wana nini wale waliokufuru wanakutumbulia (wanakukodolea) macho tu?

فَمَالِ الَّذِينَ كَفَرُوا قِبَلَكَ مُهْطِعِينَ ﴿٣٦﴾

37. Vikози-vikози (Vikosi-vikosi) kwa upande wa kulia na kwa upande wa kushoto!

عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٣٧﴾

38. Je, kila mmoja katika wao anatumai kwamba ataingizwa katika Pepo hiyo ya neema?

أَيُّضًا كُلِّ امْرِيءٍ مِنْهُمْ أَنْ يَدْخَلَ جَنَّةً يَعيِمُونَ ﴿٣٨﴾

39. Sivyo! Hakika tumewaumba kutokana na kile wanachokijua. (Maji ya uzazi. Basi ndio wataingia-Peponi tu kwa kuwa wameumbwa kwa maji ya uzazi?)

كَلَّا. إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِمَّا يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾

40. Basi naapa kwa Mola wa mashariki zote na magharibi zote kwamba sisi tunaweza

فَلَا أقيمُ رَبِّ الشَّرْقِ وَالْمَغْرِبِ إِنَّا لَقَدِيرُونَ ﴿٤٠﴾

41. Kuwabadili (na kuleta) walio bora kuliko wao; na sisi hatushindwi (na kitu).

عَلَى أَنْ يُبَدِّلَ خَيْرًا مِنْهُمْ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٤١﴾

42. Basi waache wapige porojo na wacheze, mpaka waone siku yao wanayoahidiwa

فَدَرَبُهُمْ يَخُوضُونَ وَيَلْعَبُونَ حَتَّى يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٤٢﴾

43. Siku watakapotoka makaburini kwa upesi kama kwamba wanakimbilia mfunda (mede), (mfundo wao, wanaposhindania)


يَوْمَ يُخْرِجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَانَتْهُمْ إِلَىٰ نَصْبٍ يُوقِضُونَ ﴿٤٣﴾

44. Macho yao yatainama, unyonge utawafunika. Hiyo ndiyo siku waliyokuwa wakiahidiwa.

خَاشِعَةً أَبْصَارُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ذَٰلِكَ الْيَوْمِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٤٤﴾

38,39. Wanasimangwa makafiri na wanaondoshewa tamaa yao hiyo ya kutumai kuiwa Peponi bila ya kufanya amali njema.

43. Makadiyani Katika Aya waliyofanya ya 44 wamegeuza muradi wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anataja hapo yatakayotokea Kiama, wao wanasema yametokea Makka. Wao hamu yao kumpinga Mungu tu kwa ya kweli aisemayo!



Ina Aya 28

SURAT NUH  
(Imeteremka Makka)

Ina Makara 2

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Hakika sisi tulimtuma Nuhu kwa watu wake, ya kwamba waonye watu wako kabla ya kuwajia adhabu iumizayo.

إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ أَنْ أَنْذِرْ قَوْمَكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ①

2. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni Mwonyaji niliye dhahiri kwenu

قَالَ يَقَوْمِ إِنِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُبِينٌ ②

3. Ya kuwa Muabuduni Mwenyezi Mungu na Mcheni na mnitii

إِنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ وَأَطِيعُوا أَمْرًا

4. Atakusameheni madhambi yenu na atakuahirisheni (bila ya balaa) mpaka muda uliowekwa. Hakika ijapo ajali itokayo kwa Mwenyezi Mungu haizuiliki. Laiti mngejua!

يَعْفُرْ لَكُمْ مِنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُخَذِّكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ③  
إِنِ أَجَلَ اللَّهُ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ لَوْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ④

5. Akasema: Ee Mola wangu! Kwa hakika nimewalingania, (nimewaita) watu wangu usiku na mchana

قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا ⑤

6. Lakini mwito wangu haukuwazidishia ila kukimbia;

فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَائِي إِلَّا فِرَارًا ⑥

7. Na kila mara nilipowaita Uwasamehe, waliziba mashikio yao kwa vidole vyao, na walijifunika nguo zao (gubigubi), na walizidi kuendelea (na kufuru) na wakafanya kiburi kingi.

وَإِنِّي كُلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِتَغْفِرَ لَهُمْ جَعَلُوا أَصَابِعَهُمْ فِي آذَانِهِمْ وَاسْتَعْصَمُوا بِأَنفُسِهِمْ وَأَصْرُوا وَاسْتَكْبَرُوا ⑦  
اسْتِكْبَارًا ⑧

8. Tena niliwaita kwa jahari

ثُمَّ إِنِّي دَعَوْتُهُمْ جَهْرًا ⑨

9. Kisha nikawatangazia kwa kelele; tena nikasema nao kwa siri.

ثُمَّ إِنِّي أَعَلَلْتُ لَهُمْ وَأَسْرَرْتُ لَهُمْ إِسْرَارًا ⑩

10. Nikawaambia: Ombeni msamaha kwa Mola wenu. Hakika yeye ni Mwingi wa msamaha

فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا ⑪

11. Atakuleteni mawingu yanyeshayo mvua nyingi

يُرْسِلُ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا ⑫

1. Kinatajwa kisa cha Nabii Nuhu kwa urefu na kazi ngumu kabisa aliyoifanya kwa muda wa miaka 950 mfululizo; kama ilivyobainishwa katika Aya ya 14 ya *Suratul Ankabut*. Basi tusichoke katika kufundisha mema hata ikiwa hatuioni upesi natija yake. Natija itakuja tu.

12. Na atakupeni mali na watoto, na atakupeni mabustani, na atakufanyieni mito.

13. Mumekuwaje hamuweki hishima ya Mwenyezi Mungu.

14. Na hali yeye amekuumbeni namna baada ya namna?

15. Je, hamuoni jinsi Mwenyezi Mungu alivyoziumba mbingu saba tabaka-tabaka (moja juu ya moja)

16. Na akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru na akalifanya jua kuwa taa?

17. Na Mwenyezi Mungu amekuotesheni katika ardhi, (kama) mimea

18. Kisha atakurudisheni humo na atakutoeni tena.

19. Na Mwenyezi Mungu amekufanyieni ardhi kuwa (kitu kizuri) mlichotandikiwa

20. Ili mtembee humo katika njia zilizo pana.

21. (Nabii) Nuhu akasema: Mola wangu! Hakika hao wameniasi na wamewafuata ambao mali yao na watoto wao hawakuwazidishia ila hasara.

22. Na wakafanya hila kubwa kubwa (za kubatilisha dini).

23. Na ambao waliwaambia (wafuasi wao): 'Msiache miungu yenu, wala msiwache Waddi wala Suwaa wala Yaghutha Wala Yauka wala Nasra.' (Majina ya waungu wao wa kisanamu).

24. Nao wamekwishapoteza (watu) wengi; wala usiwazidishie madhalimu hawa ila kupotelea mbali!

25. Basi kwa ajili ya makosa yao waligharikishwa wakaingizwa Motoni, wala hawakuwapata wa kuwanusuru mbele ya Mwenyezi Mungu.

26. Na Nuhu (akazidi) kusema: Mola wangu! Usimuache juu ya ardhi mkazi wake yoyote katika makafiri.

27. Hakika ukiwaacha watapoteza watu wako (waliotengenea) wala hawatazaa ila (watoto) waovu wenye kufuru (kama wao).

وَمِمَّا كَرِهَ اللَّهُ لَنَا ذَلِكُمْ وَإِنَّ رَبَّنا لَخَبِيرٌ  
بِذُنُوبِكُمْ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ۝١٢

مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ۝١٣

وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ۝١٤

أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ۝١٥

وَجَعَلَ الْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسُ سِرَاجًا ۝١٦

وَاللَّهُ أَنْتَبَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ بَنَاتًا ۝١٧

ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا وَيُرْجِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا ۝١٨

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ بِسَاطًا ۝١٩

لِتَسْلُكُوا مِنْهَا سُبُلًا فِجَاجًا ۝٢٠

قَالَ نُوحٌ رَبِّ إِنَّهُمْ عَصَوْني وَاتَّبَعُوا مَنْ لَمْ

يَزِدْهُ مَالًا وَوَلَدًا إِلَّا خَسَارًا ۝٢١

وَمَكَرُوا مَكْرًا كَبِيرًا ۝٢٢

وَقَالُوا لَا تَنْزِلُنَا إِلَّا سَمَاءٌ مِّنْ سَافِلَةٍ ۝٢٣

وَمَا نُنزِلُ إِلَّا الْمَوْتَ وَالْحَقَّ وَالْحَقَّ ۝٢٤

وَقَدْ أَضَلُّوا كَثِيرًا ۝٢٥ وَلَا تَزِدِ الظَّالِمِينَ

إِلَّا ضَلَالًا ۝٢٦

مِمَّا خَطَبْتَهُمْ أُعْرِفُوا فَادْخُلُوا نَارًا ۝٢٧

يَجِدُوا لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْصَارًا ۝٢٨

وَقَالَ نُوحٌ رَبِّ لَا تَذَرْنِي عَلَى الْأَرْضِ مِنْ


الْكٰفِرِينَ دَرِيًّا ۝٢٩

إِنَّكَ إِن تَذَرَهُمْ يُضِلُّوا عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوا

إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ۝٣٠

28. Mola wangu! Nighufirie mimi na wazee wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu hali ya kuwa ni Mwislamu, na Waislamu wanaume na Waislamu wanawake; wala usiwazidishie madhalimu ila maangamizo.

رَبِّ اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَنْ دَخَلَ بَيْتِي  
 مُؤْمِنًا وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ، وَلَا تَزِدِ  
 الظَّالِمِينَ إِلَّا تَبَارَكَ اللَّهُ



Ina Aya 28

**SURATUL JINN**  
(Imeteremka Makka)

Inu Makaru 2

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikia (Qurani) likasema: 'Hakika tumesikia Qurani ya ajabu

قُلْ أُوْحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْمَمَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا ۝

2. 'Inaongoza katika uongofu; kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yoyote tena na Mola wetu

يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ وَلَنْ نُشْرَكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا ۝

3. 'Na kwa hakika utukufu wa Mola wetu umetukuka kabisa, hakujifanyia mke wala mwana

وَأَنَّهُ تَعَلَّى جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَلَا وَلَدًا ۝

4. 'Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikuwa wakisema maneno yaliyopindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu

وَأَنَّهُ كَانَ يَفُولُ سَفِيهُنَا عَلَى اللَّهِ شَطَطًا ۝

5. 'Nasi tulikuwa tukidhani ya kuwa watu na majini hawatasema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu

وَأَنَّا ظَنَنَّا أَن لَّن نَقُولَ الْإِنسَ وَالْجِنُّ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۝

6. 'Na hakika kulikuwa na wanaume miongoni mwa wanaadamu wakijikinga kwa wanaume miongoni mwa majini; kwa hivyo wakawazidishia taklifu; (kama hivi wenye pepo wakataka hao mapepo kuchezewa ngoma na kuchinjiwa wanyama)

وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ۝

7. 'Na kwa hakika wao walidhani kama mlivyodhani nyinyi ya kuwa Mwenyezi Mungu hataleta (Mtume) yoyote.

وَأَنَّهُمْ ظَلَمُوا كَمَا ظَلَمْتُمْ أَن لَّن نَّبْعَثَ اللَّهَ أَحَدًا ۝

8. 'Nasi tulizigusa mbingu (tulikwenda mbinguni) tukazona zimejaa walinzi wenye nguvu na nyota (zing'arazo)

وَأَنَّا لَمَسْنَا السَّمَاءَ فَوَجَدْنَاهَا مُلْتَأَتٍ حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهَبًا ۝

1. Tumetaja habari yao katika Aya ya 29 ya *Suratul Ahqaf*. Hapa inatajwa kwa urefu.

Makadiyani Wamepindua vile vile maana ya Jini kama walivyopindua katika Qurani yote nzima ya Mwenyezi Mungu. Na tuliwajibu katika marejezo ya Aya ya 111 ya *Suratul An-am*, na katika Aya nyingine za Sura hii, na katika *Suratul Aaraf* na nyinginezo. Wao raha yao ni kumpinga Mwenyezi Mungu kwa anayoyasema, na kumpinga Mtume wake. Mtume amewambia Majini khasa, kama alivyosema Mwenyezi Mungu. Wao wanasema hao ni Mayahudi. Hawampati mfasiri yoyote, wa Qurani aliyesema kuwa hao walikuwa si Majini ila ni Mayahudi.

7. na 26. Katika hizi Aya walizozifanya za 8 na 27 wametambalia tena kumdaia Utume huyo mtu wao wenyewe peke yao.

9. 'Na hakika tulikuwa tukikaa humo katika baadhi ya makao ili kusikiliza; lakini anayetaka kusikiliza sasa atakuta kimondo (kijinga cha moto) kinamvizia

10. 'Nasi hatujui kama wanatakiwa shari wale wanaokaa katika ardhi au Mola wao anawatakiwa uwongofu (kheri).

11. 'Na hakika katika sisi wako wema na wengine katika sisi ni kinyume cha hayo: tumekuwa njia mbali mbali

12. 'Nasi tulijua ya kuwa hatuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu katika nchi wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia (katika mbingu)

13. 'Nasi tulipousikia uwongofu tuliuamini; basi anayemuamini Mola wake hataogopa kupunjwa wala kutwikwa (kubebeshwa) dhambi (za mtu mwengine)

14. 'Nasi wamo miongoni mwetu waliosilimu na wamo miongoni mwetu wanaokengeuka Waliosilimu hao ndio waliotafuta uwongofu

15. 'Na wanaokengeuka hao watakuwa kuni za Jahanamu.'

16. Na kama wanalishika kwa imara njia (iliyonyoka) tungaliwanyesha maji kwa wingi, (yaani tungeliwastarehesha).

17. Ili tuwajaribu; (tuwafanyie mtihani) kwa hayo. Na anayepuuza kumkumbuka Mola wake atamsukuma katika adhabu ngumu

18. Na kwa hakika misikiti (yote) ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yoyote pamoja na Mwenyezi Mungu

19. Na hakika mja wa Mwenyezi Mungu (Nabii Muhammad) aliposimama kumuomba (Mola wake mmoja tu) walikuwa karibu kumuangukia (wamuangamize kwa kuhamaki kwao).

20. Sema: "Ninamuabudu Mola wangu tu wala simshirikishi na yoyote."

21. Sema: "Mimi sikumilikiini kukudhuruni wala kukuongoweni."

وَأَنَّا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقَاعِدَ لِلسَّمْعِ ، فَمَنْ يَسْمَعُ الْآنَ يَجِدْ لَهُ شَيْئًا يَصْدًا ۝

وَأَنَّا لَا تَدْرِي أَسْرَأُيُودُ بِنِّ فِي الْأَرْضِ أَمْ أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ۝

وَأَنَّا مِنَّا الضَّالُّونَ وَمِنَّا دُونَ ذَلِكَ كُنَّا طَرَائِقَ قِدَدًا ۝

وَأَنَّا ظَنَنَّا أَن لَنْ نَحْجِزَ اللَّهَ فِي الْأَرْضِ وَلَنْ نَحْجِزَهُ هَرَبًا ۝

وَأَنَّا لَبِئْسَ سَمْعَنَا الْهُدَىٰ أَمَّا بِهِ ، فَمَنْ يُؤْمِنُ ، بِرَبِّهِ فَلَا يَنَافُ بِخَسَاءٍ وَلَا رَهَقًا ۝

وَأَنَّا مِنَّا الْمُسْلِمُونَ وَمِنَّا الْقَاسِطُونَ ، فَمَنْ أَسَٰمَ فَأُولَٰئِكَ تَحَرَّوْا رَشَدًا ۝

وَأَمَّا الْقَاسِطُونَ فَكَانُوا لِجَهَنَّمَ حَطَبًا ۝

وَأَن لَّوِ اسْتَقَامُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ لَأَسْقَيْنَهُمْ مَّاءٍ غَدَقًا ۝

لِنَقْتَبَهُمْ فِيهِ ، وَمَنْ لِّعَرَضٍ عَن ذِكْرِ رَبِّهِ يَسْلُكْهُ عَذَابًا صَعَدًا ۝

وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ۝


وَأَنَّهُ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ۝ عَلَيْهِ لَبَدًا ۝

قُلْ إِنَّمَا أَدْعُوا رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِهِ أَحَدًا ۝

قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا رَشَدًا ۝

19-25. Tazama yaliyomfika Mtume na namna alivyokuwa akiwajibu. Basi usishtuke kwa vishindo vitakavyokufika katika kulingania kheri na kukataza shari, na jawabu yako iwe kama hii ya Mtume.





Inu Aya 20

**SURATUL MUZZAMMIL**

Inu Makura 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneernesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneernesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Ewe uliyejifunika maguo!
2. Simama usiku (kucha kufanya ibada); ila muda mdogo (tu hivi).
3. Nusu yake au ipunguze kidogo
4. Au izidishe — na soma Qurani vilivyo.
5. Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito.
6. Hakika kuamka usiku (na kufanya ibada) kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno (yake) yanatuwa zaidi.
7. Hakika mchana una shughuli nyingi.
8. Na litaje jina la Mola wako na ujitupe kwake kwa kweli. (Usitafute mizimu wala uchawi wala . . .)
9. (Yeye ndiye) Mola wa mashariki na magharibi — hakuna muabudiwa ila Yeye, basi mfanye kuwa mlinzi (wako).
10. Na subiri juu ya hayo wasemayo (hao makafiri) na uwaepuke mwepuko mwema.
11. Na niache mimi na hao wanaokadhibisha walionemeka, na uwape muhula (muda) kidogo (tu hivi).

يَا أَيُّهَا الْمُرْسَلُ  
 قُمْ اللَّيْلَ إِلَّا قَلِيلًا  
 بَصِّصْهُ أَوْ انْقُصْ مِنْهُ قَلِيلًا  
 أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا  
 إِنَّا سَأَلْنَا عَلَيْكَ لَوْلَا تَقِيْلًا  
 إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْأً وَأَقْوَمُ قِيْلًا  
 إِنَّكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيْلًا  
 وَادْكُرْ اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَبْتِيْلًا  
 رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ  
 وَكِيْلًا  
 وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَاهْجُرْهُمْ هَجْرًا جَمِيْلًا  
 وَذَرْنِي وَ الْمُكَذِّبِينَ أُولِي النَّعْمَةِ وَمَهِّلْهُمْ قَلِيْلًا

1. Waarabu walikuwa wana dasturi ya utani na kupeana majina ya mafumbo kwa jambo dogo tu hili mtu analolifanya. Na Qurani imeteremka kwa msemo wa Kiarabu.

Mtume pale mwanzo ulipomjia Wahyi alishtuka, akarejea kwa Bibi Khadija na homa ya Nderema (ya kitapo) anatemeka. Akamwambia huyo Bibi "Nifunike nguo kubwa." Basi Mwenyezi Mungu akamsemeza kwa jina la Utani hapa na katika Sura ya pili yake, akamwambia "Ewe uliyejifunika maguo! Simama! Jitoe katika maguo uliyojifunika. Ufanye haya sasa uliyoamrisha." Basi tamko la *Muzzammil* lililo katika Sura hii ni sawa sawa na tamko la *Muddaththir* lililo katika Sura ya pili yake.

2. Mwanzo wa Uislamu — kabla ya kuwako mambo mengi ya kufanya — walihimizwa kukithirisha Ibada. Kisha zikapunguzwa kwa sababu zilizotajwa hapo katika Aya ya 20.

Na mwanzo wa Sura hii na mwanzo wa Sura ya pili yake ni katika Sura za mwanzo kabisa; na hiyo *Suratul Muddaththir* ndiyo Sura ya pili khasa japokuwa imewekwa mahala pa Sura ya 74.

12. Hakika tuna (namna namna ya) adhabu na Moto uwakao (kwa ukali kabisa)

13. Na chakula kikwamacho (kisakamacho) kooni na adhabu iumizayo.

14. Katika siku ambayo ardhi na milima itakapotetemeka, na milima itakuwa kama mkusanyiko wa mchanga usiojishika.

15. Hakika sisi tumekuleteeni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama tulivyompeleka Mtume kwa Firauni.

16. Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi tukamtesa mateso makubwa.

17. Basi nyinyi mkikufuru, mtawezaje kujihifadhi na (balaa ya) siku ambayo itawafanya watoto kuwa wenye kutoka mvi (wazee)?

18. Mbingu zitapasuka (siku) hiyo; ahadi yake (Mwenyezi Mungu) itatekelezwa tu.

19. Kwa hakika hii (Qurani) ni mawaidha, basi anayetaka atajifanyia njia (nzuri ya kwenda) kwa Mola wake.

20. Kwa hakika Mola wako anajua kuwa wewe unasimama (kumuabudu Mwenyezi Mungu) karibu na thuluthi mbili za usiku; na (engine) nusu yake, na (wakati mwingine) thuluthi yake; na baadhi ya watu walio pamoja nawe (wanafanya haya pamoja nawe), na Mwenyezi Mungu ndiye anayepanga vizuri kadiri ya urefu wa usiku na mchana. Anajua kuwa huwezi kufanya hivyo, basi amekusameheni; kwa hivyo someni kiasi kinachosahilika tu kwenu katika Qurani. Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa na wengine watasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila ya Mwenyezi Mungu, na wengine watapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa hivyo someni kilicho sahali humo. Na simamisheni Sala na toeni Zaka, na Mkatieni Mwenyezi Mungu sehemu njema (katika mali yenu iwe ndiyo Zaka na sadaka na . . .). Na kheri yoyote mnayoitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu imekuwa bora zaidi na ina thawabu kubwa sana. Na ombeni msamaha kwa Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

15. Katika Aya waliyoifanya kuwa ya 16 wametia chungu ya farumu ya uwongo ya kumdaia. Utume huyo mtu wao. Tazama marejezo yetu katika marejezo ya Aya ya 40 ya Suratul Ahzaab.

إِنَّ لَدَيْنَا أَنْكَالًا وَجَحِيمًا ۝

وَلَطَعَامًا ذَا غُصَّةٍ وَعَذَابًا أَلِيمًا ۝

يَوْمَ تَرْجُفُ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ وَكَانَتِ الْجِبَالُ كَغِيَابٍ مَهِيلاً ۝

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا دَاعِيًا إِلَى الْإِسْلَامِ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَى فِرْعَوْنَ رَسُولًا ۝

فَعَصَى فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلاً ۝

فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِنْ كَفَرْتُمْ يَوْمًا يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا ۝

السَّمَاءُ مُنْقَطِرَةٌ بِهِ كَانَتْ وَعْدُهُ مَفْعُولًا ۝

إِنَّ هَذِهِ تَذَكُّرَةٌ ۚ فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ۝

إِنَّ رَبَّكَ يَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدْنَىٰ مِنْ ثُلُثِي اللَّيْلِ وَنِصْفَهُ وَثُلُثَهُ وَطَائِفَةٌ مِّنَ الَّذِينَ مَعَكَ ۚ

وَاللَّهُ يَقْدِرُ اللَّيْلَ وَ النَّهَارَ ۚ عَلِمَ أَن لَّنْ

نُحْصِيَهُ فَتَابَ عَلَيْكُمْ فَاقْرَءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنَ الْقُرْآنِ ۚ عَلِمَ أَن سَيَكُونُ مِنكُمْ مَّرْضَىٰ ۚ

وَآخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَلْتَمِتُونَ مِن


فَضْلِ اللَّهِ ۚ وَآخَرُونَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۚ فَاقْرَءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ ۚ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا

الزَّكَاةَ وَاقْرَءُوا لِلَّهِ قَرْضًا حَسَنًا ۚ وَمَا تُقَدِّمُوا

لَا نُفْسِكُمْ مِنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرٌ

وَأَعْظَمُ أَجْرًا ۚ وَاسْتَغْفِرُوا لِلَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ

رَحِيمٌ ۝



Ina Aya 56

## SURATUL MUDDATHHIR

Ina Makara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuncemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Ewe uliyejifunika maguo
2. Simama uonye (viumbe)
3. Na Mola wako umtukuze
4. Na nguo zako uzisafishe
5. Na Mabaya yapuuze, (endelea kuyapuuza)
6. Wala usiwafanyie ihsani (viumbe) ili upate kujikithirishia (wewe hapa duniani)

يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ ۝

قُمْ فَأَنْذِرْ ۝

وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ ۝

وَتُوبَاكَ فَطَهِّرْ ۝

وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ۝

وَلَا تَنْتِنْ لَنْتَنِكُمْ ۝

7. Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira (kwa kila yatakayokufika).

وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ۝

8. Litakapogwa parapanda (la Kiama)
9. Siku hiyo itakuwa siku ngumu
10. Kwa makafiri; haitakuwa nyepesi.
11. Niache mimi na niliyemuumba peke yangu
12. Na nikamjaalia awe na mali nyingi
13. Na watoto waonekanao (kila mahala)

فَإِذَا نُفِرَ فِي النَّاقُورِ ۝

فَذَلِكَ يَوْمٌ عَسِيرٌ ۝

عَلَى الْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ۝

ذُرِّيَّيْ وَمَنْ خَلَقْتُ وَجِيدًا ۝

وَجَعَلْتُ لَهُ مَالًا مَمْدُودًا ۝

قَبْرَيْنِ شُهُودًا ۝

14. Na nikamtengenezea mambo yake kumtengenezea (kuzuri kabisa)

وَمَهَّدْتُ لَهُ تَمْهِيدًا ۝

15. Kisha anatumaini nimzidishie!
16. Wapi! Hakika yeye alikuwa anazipinga Aya zetu.

ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ ۝

كَلَّا إِنَّهُ كَانَ لِإِيْتِنَا عَنِيدًا ۝

17. Basi nitamtesa kwa mateso makuu.

سَأَرْهُقُهُ صَعُودًا ۝

11-26. Anahadidiwa yule mpingaji mkubwa kabisa wa Uislamu mwanzo kabisa ulipokuja Uislamu. Naye ni Walyd bin Al Mughyra, ami yake Abu Jahl. Na jina khasa la Abu Jahl ni Amr bin Hisham bin Al Mughyra. Nyumba hii mwanzo wa Uislamu ilikuwa ya uadui mkubwa kabisa usiokuwa na mfano juu ya Waislamu na Uislamu. Na mwisho wake ikawa katika nyumba za kani kubwa za kuupigania Uislamu. Majenerali hawa mashuhuri wa Kiislamu — Khalid bin Walid, Ikrima bin Jahl, Harith bin Hishaam na wengineo — wanatokana na nyumba hii.



34. Na kwa asubuhi inapopambazuka وَالصَّبْحِ إِذَا اسْفَرَ ۝
35. Hakika huo (Moto) ni moja katika (balaa) kubwa (kabisa) إِنَّهَا لَاحَدُ الْكَبِيرِ ۝
36. Ni onyo kwa binadamu نَذِيرًا لِلْبَشَرِ ۝
37. Kwa anayetaka miongoni mwenu kutakadamu (kwenda mbele) au kutaakhari (kurejea nyuma). لِمَنْ سَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَسْتَقْدِمَ أَوْ يَتَأَخَّرَ ۝
38. Kila nafsi itafungika (Motoni) kwa (amali mbovu) ilizozichuma كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ۝
39. Isipokuwa watu wa kuliani (watu wa kheri) إِلَّا أَصْحَابُ الْيَمِينِ ۝
40. (Hao watakuwa) katika Mabustani, wawe wanaulizana فِي جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۝
41. Juu ya watu wabaya (wawaambie): عَنِ الْمَجْرِمِينَ ۝
42. "Ni kipi kilichokupelekeni Motoni?" مَا سَأَلْتُمْ فِي سَعْرٍ ۝
43. Waseme: "Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakisali" قَالُوا لَمْ نَكُ مِنَ الْمَصْلُوبِينَ ۝
44. "Wala hatukuwa tukilisha maskini" وَلَمْ نَكُ نَطْعِمُ الْيَسْكِينِ ۝
45. "Na tulikuwa tukizama (katika maasia) pamoja na waliokuwa wakizama" وَكُنَّا نَحْمِلُ مَعَ الْخَائِضِينَ ۝
46. "Na tulikuwa tukikadhibisha siku ya hukumu" وَكُنَّا نُكَذِّبُ بِيَوْمِ الدِّينِ ۝
47. "Mpaka mauti yakatujia." حَتَّىٰ آتَانَا الْيَقِينَ ۝
48. Basi hautawafaa uombezi wa waombezi (wowote wale). فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشُّفْعَاءِ ۝
49. Basi wana nini? Wanapuuza onyo hili! فَمَا لَهُمْ عَنِ التَّذْكَرَةِ مُعْرِضِينَ ۝
50. (Wanakwenda mbio ili wasisikie onyo hili) Kama kwamba ni mapunda, wanaokwenda mbio كَانَتْ حُمْرٌ مُسْتَنْفِرَةٌ ۝
51. Wanaokimbia simba! فَزَلَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ ۝
52. Ati kila mmoja katika wao anataka apewe nyaraka zitakazofunuliwa (Siku ya Kiama; za Amali zao zilizoandikwa na Malaika — wanafanya stihzai kwa kutaka haya tangu sasa) بَلْ يَرِيدُ كُلُّ امْرِئٍ مِنْهُمْ أَنْ يُؤْتَىٰ صُحُفًا مُنشَرَةً ۝
53. Sivyo, bali wao hawaiogopi Akhera. كَلَّا بَلْ لَا يَخَافُونَ الْآخِرَةَ ۝
54. Sivyo hivyo. Kwa haika huo ni ukumbusho. كَلَّا إِنَّهُ تَذَكُّرٌ ۝

43-55. Zinatajwa baadhi ya sababu za kuwapelekea watu kuingia Motoni.


55. Basi anayetaka atakumbuka (na asiyetaka basi).

56. Na hawatakumbuka isipokuwa apende Mwenyezi Mungu: Yeye ndiye anayestahiki kuogopwa, na Mwenye kusamehe.

فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ۗ

وَمَا يَذْكُرُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ هُوَ أَهْلُ التَّقْوَىٰ

وَأَهْلُ الْمَغْفِرَةِ ۗ



Ina Aya 40

## SURATUL QIYAMAH

Ina Makkara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuncemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa siku ya Kiama
2. Tena naapa kwa nafsi inayojilaumu; (kuwa mtafufuliwa na mtalipwa).
3. Anadhani mtu ya kuwa sisi hatutaikusanya mifupa yake?
4. Kwa nini! Sisi tunaweza (hata) kuzisawazisha ncha za vidole vyake (tutakapomfufua mara ya pili, ziwe kama zilivyokuwa duniani).
5. Lakini mtu anataka tu kuyakataa yaliyo mbele yake (ili ajipe moyo kuwa hakuna kitu huko Akhera, azidi kufanya maovu).

لَا أُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ ۝

وَلَا أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ۝

أَيَحْسَبُ الْإِنْسَانُ أَنْ نَبْنَعَهُ عِظَامَهُ ۝

بَلَىٰ قَدِيرِينَ عَلَىٰ أَنْ نُسَوِّيَ بَنَانَهُ ۝

بَلْ يُرِيدُ الْإِنْسَانُ لِيَفْجُرَ أَمَامَهُ ۝

6. Anauliza: (kwa shere) "Itakuwa lini hiyo siku ya Kiama?"

يَسْأَلُ أَيَّانَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۝

7. (Itakuwa siku hiyo), wakati litakapoparama jicho

فَإِذَا بَرِقَ الْبَصَرُ ۝

8. Na mwezi utakapopatwa

وَحَسَفَ الْقَمَرُ ۝

9. Na jua na mwezi vikakutanishwa (katika kupatwa)

وَجُمِعَ الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ۝

10. Mtu atasema siku hiyo: "Pa wapi mahali pa kukimbilia?"

يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُ ۝

11. (Aambiwe): "La! Hakuna mahali pa kukimbilia!"

كَلَّا لَا وَزَرَ ۝

1. Imeitwa Sura hii *Suratul Qiyama* kwa ajili ya kutajwa ndani yake habari nyingi za Kiama, si kwa ajili ya hiyo sababu walivyotaja wamirzai katika tafsiri yao.

4. Aya hii ni moja katika zile Aya zinazoonyesha ajabu ya maneno ya Qurani na kusibu kwake. Mwenyezi Mungu anasema hapa kuwa siku ya kufufuliwa viumbe atavirejesha viungo vya viumbe kama vile vilivyokuwa, sawa sawa: hata ncha za vidole vya kila mtu vitarejea kama vilivyokuwa. Sasa kiasi cha myaka mia hivi ndio watu wa Ulaya wametambua kuwa alama za ncha za vidole vya binadamu hazishabihiani — kila mtu ni namna mbali na mwenziwe. Basi Qurani imeyataja haya zamani na kusema kuwa alama za ncha za vidole vya kila mtu zitarejea kama vile zilivyokuwa. Wanataka nini mengine zaidi kuliko haya tunayoyasema kila siku ya ukweli wa maneno yaliyosemwa katika Qurani? Hayaanguki chini yaliyosemwa humo.

12. Siku hiyo marejeo ni kwa Mola wako (tu).
13. Siku hiyo ataambiwa mwanaadamu aliyoyatanguliza na aliyoyaakhrisha.
14. Bali mtu ni shahidi juu ya nafsi yake
15. Ingawa anatoa nyudhuru zake za uwongo.
16. Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka. Wewe sikiliza tu. Usiseme kitu).
17. Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha).
18. Wakati tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake.
19. Kisha ni juu yetu kuubainisha (kukubainishia).
20. Sivyo! Bali nyinyi mnapenda maisha ya hapa duniani
21. Na mnaacha (kuyashughulikia) maisha ya Akhera.
22. Nyuso (nyingine) siku hiyo zitang'ara (kweli kweli)
23. Zinamtazama Mola wao (au neema alizowapa).
24. Na nyuso (nyingine) siku hiyo zitakunjana
25. Zitajua ya kuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo.
26. Sivyo (hivi mnavyofanya)! (Roho) itakapofikia katika mitulinga (mifupa ya mabega)
27. Na kukasemwa: "Ni nani wa kumzingua (na kumpoza mgonjwa huyu)?"
28. Na mwenyewe akajua kwa hakika kuwa hiyo ni (saa ya) kufariki (dunia)

إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ﴿١٢﴾  
يَكْتُبُوا الْإِنْسَانَ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿١٣﴾

بَلِ الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ ﴿١٤﴾  
وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ﴿١٥﴾

لَا تُحْرِكُ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿١٦﴾

إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ﴿١٧﴾

فَإِذَا قَرَأَهُ فَأَنبِئْهُ قُرْآنَهُ ﴿١٨﴾

ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ﴿١٩﴾

كَلَّا بَلِ تُحِبُّونَ الْعَاجِلَةَ ﴿٢٠﴾

وَتَذُرُونَ الْآخِرَةَ ﴿٢١﴾

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ لَّا ضَرَّةَ ﴿٢٢﴾

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾

وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ بَاسِرَةٌ ﴿٢٤﴾

تَظُنُّ أَنْ يُفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ﴿٢٥﴾

كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ الشَّرَاقِيَ ﴿٢٦﴾

وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ ﴿٢٧﴾

وَوَظَنَّ أَنَّهَ الْفِرَاقُ ﴿٢٨﴾

16. Mtume ilivyokuwa hajui kuandika wala kusoma kilichoandikwa, alifanya khofu kubwa kabisa kwa kuona ataichibiti vipi hiyo Qurani itakayokuwa anateremshiwa, kila siku Chungu ya Aya nyingine nyingine. Ndio anaambiwa asifanye khofu hata chembe. Mwenyezi Mungu atamwezesha kuhifadhi papo hapo kila anachotamkiwa na Jibrili wala asisahau maisha yake. Basi akawa kama alivyoambiwa.

16-19. Mwisho wa maelezo ya Aya walizozipa nambari hizi 17-20 wametia kule (a) kumdaia Utume mtu wao. Na tumejibu sana habari hii. Na wametia (b) kukataa Naskh. Na haya tumeyataja katika marejezo ya Aya ya 106 ya *Suratul Baqarah*.

29. Na utakapoambatanishwa muundi kwa muundi

30. Siku hiyo ni kuchungwa (tu) kupelekwa kwa Mola wako.

31. Hakusadiki wala hakusali

32. Bali alikadhibisha na akarudi nyuma

33. Kisha alikwenda kwa watu wake, na huku akiringa.

34. (Ataambiwa): "Imekwisha kukufika (adhabu ya Mwenyezi Mungu); imekwisha kukufika"

35. Kisha "Imekwisha kukufika (adhabu ya Mwenyezi Mungu); imekwisha kukufika."

36. Je! Anafikiri binadamu kuwa ataachwa bure, (asipewe amri za Mwenyezi Mungu wala makatazo yake)?

37. Je! Hakuwa tone la manii lililotonwa?

38. Kisha akawa kidonge cha damu, kisha akamuumba na akamsawazisha (mwanaadamu kamili)?

39. Kisha akamfanya namna mbili, mwanamume na mwanamke.

40. Je! Hakuwa Huyu ni Muweza wa kuhuisha wafu?

وَ اتَّخَذَتِ السَّاقُ بِالسَّاقِ ۞  
إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمَسَاقُ ۞

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّىٰ ۞

وَلَكِنَّ كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ۞

ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰ آهَالِهِ يَمُوتُ ۞

أَوَّلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ ۞

ثُمَّ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ ۞


أَيَحْسَبُ الْإِنْسَانُ أَنْ يُتْرَكَ سُدًىٰ ۞

أَلَمْ يَكُن لُّطْفَةً مِنِّي يَتَوَكَّلُ ۞

ثُمَّ كَانَ عَاقِبَةُ فِخْلِكَ فَسُوءُ ۞

فَجَعَلَ مِنْهُ الرُّوحَيْنِ الذَّكَرَ وَ الْاُنْثَىٰ ۞

يَعِجُّ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِرٍ عَلَيَّ أَنْ يُبْجِزَ الْمَوْتَىٰ ۞



Ina Aya 31

SURATUD DAHR

Ina Makara 2

(Imeteremka Madina)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Hakika ulimpitia Binaadamu wakati mrefu katika dahari, hakuwa kitu kinachotajwa. (Binaadamu ndiye kiumbe cha mwisho kuletwa ulimwenguni).

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُنْ سَيِّئًا مَّذْكَورًا ①

2. Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: (ya mwanamume na mwanamke), ili tumfanyie mtihani (kwa amri zetu na makatazo yetu); kwa hivyo tukamfanya ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِّنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ①

3. Hakika sisi tumemuongoa, (tumembainishia) njia (zote mbili hizi; kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukurani au awe mwenye kukufuru, (kukanusha).

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ①

4. Hakika sisi tumewaandalia, (tumewawekea tayari) makafiri minyororo na makongwa na Moto mkali.

إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَلَاسِلًا وَأَغْلَالًا وَسَعِيرًا ①

5. Hakika watu wazuri watakunywa kinywaji kilichochanganyika na kafuri.

إِنَّ الْآبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِمَّنْ كَانُوا كَاذِبِينَ ①

1. Watu wanaifanya Sura hii ndiyo ya kuondosha Nadhiri, basi siku ya kuondosha sharti isomwe Sura hii ndiyo ionekane kuwa "Nadhiri imekwishaondoka." Na haya ni uzushi tu wala hapana habari hii.

Na hili jambo la kuweka nadhiri tunalolifanya, kama hivi kusema: "Nikizaa nitafanya. . . au Nikipata kazi . . . au Nikisalimika katika . . ." Hili si jambo lililosuniwa wala si la kumpa mtu thawabu. Hivi inakuwa kama unalipana na Mwenyezi Mungu: "Ukinifanyia hivi na mimi nitafanya hivi." Basi hili si Jambo linalopendwa na dini, kama alivyosema Mtume katika Hadithi zake zilizo sahihi. Bali akilikataza na akisema kufanya hivi ni sababu tu ya bakhili kutoa kitu chake. Hadithi hii imetajwa na Maimamu wakubwa wa Hadithi wote.

Nadhiri iliyo nzuri ni kupata analolitaka, ukatoa sadaka kwa ajili ya kushukuru hiyo neema aliyokupa; siyo kuagana na Mungu tangu mbele kuwa ukinipa nitakupa.

Na hizo nadhiri zako ulizokwisha kuziweka, ziondoshe kama ulivyoweka lakini usifanye tena.

Mwanzo wa Sura hii wamepindua muradi wa Mwenyezi Mungu. Nao ni kutaja kuumbwa Mtu wa mwanzo — Nabii Adamu. Wao wanampinga Mwenyezi Mungu — kama tulivyowarejeza katika marejezo ya Aya ya 30 *Suratul Baqarah* — wanasema Nabii Adamu siye mtu wa mwanzo. Ndiyo katika mwanzo wa Sura hii wakapindua muradi wa Mwenyezi Mungu wakasema: "na inaeleza juu ya mtu kufika ukamilifu ambao ndio kusudi la kuumbwa kwake." Wanamfuata Darwin kuwa binadamu asili yao walikuwa makima!

5. Labda mshembeli. Kwa kihindi unaitwa Chamfar na kafuri, kwa kiingereza Camphor.

5-22. Wanatajwa wema na watakayoyapata.

6. (Hiyo kafuri) ni mto watakaounywa waja wa Mwenyezi Mungu; watautiririsha mtiririsho (mzuri namna watakavyo).

7. (Watu hao ni hawa) wanaotimiza wajibu (wao) na wanaoigopa siku ambayo shari yake itaenea (sana).

8. Na huwalisha chakula maskini na mayatima na wafungwa, na hali ya kuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho).

9. (Husema wenyewe katika nyoyo zao wanapowapa chakula hicho): "Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu (tu) hatutaki kwenu malipo wala shukurani."

10. "Hakika sisi tunaigopa kwa Mola wetu hiyo siku yenye shida na taabu."

11. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha.

12. Na atawajazi Mabustani (ya Peponi) na maguo ya hariri, kwa sababu ya kusubiri (kwao)

13. Humo wataegemea viti vya enzi, hawataona humo jua (kali) wala baridi (kali).

14. Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yake yataning'inia mpaka chini.

15. Na watapitishiwa vyombo vya fedha na vikombe vya vigae

16. Vigae vya fedha; wamevijaza kwa vipimo.

17. Na humo watanyweshwa kinywaji kilichochanganyika na tangawizi.

18. Huo ni mto ulio humo (Peponi) unaitwa Salsabili.

19. Na watawazungukia (kuwatumikia), wavulana wasiochakaa, ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizotawanywa.

عَيْنَا يُثْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ①

يُوفُونَ بِاللَّذْرِ وَيَتَأَفُونَ يَوْمًا كَانَ شَرًّا  
مُسْتَطِيرًا ②

وَ يُطْعَمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِمْ مَسْكِينًا وَ يَتِيمًا  
وَ أَسِيرًا ③

إِنَّا نَظْمِعُكُمْ لَوَجْهِ اللَّهِ لَا تَرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَ لَا  
شُكْرًا ④

إِنَّا نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ⑤

فَوَقَّهُمُ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَّاهُمْ نَصْرَةً  
وَ سُورًا ⑥

وَ جَزَاهُمْ بِمَا صَبَرُوا جَنَّةً وَ حَرِيرًا ⑦

مُتَّكِنِينَ فِيهَا عَلَى الْأَرْكَانِ، لَا يَرَوْنَ فِيهَا  
شَسًّا وَ لَا زَهْرِيرًا ⑧

وَ دَابِيبَةً عَلَيْهِمْ ظِلُّهَا وَ ذُلَّتْ قُطُوفُهَا  
تَدْلِيلًا ⑨

وَ يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِإِينَةٍ مِنَ فَضَّةٍ وَ  
أَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيرًا ⑩

قَوَارِيرًا مِنْ فِضَّةٍ قَدَرُوهَا تَقْدِيرًا ⑪

وَ يُتَّقُونَ فِيهَا كَأَسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَنْجَبِيلًا ⑫

عَيْنًا فِيهَا تُسَمَّى سَلْسَبِيلًا ⑬

وَ يُطَوَّفُ عَلَيْهِمْ وَ لَدَانٌ مُخَلَّدُونَ، إِذَا  
رَأَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَنُورًا ⑭

17-18. Katika Aya waliyoifanya ya 18 wanaona kuwa Mwenyezi Mungu anataja starehe za Akhera na mifano ya vinywewa vya humo; wao wamepindua chini juu; wamesema—katika maelezo yao— "Zanjabyl = Wapanda Jabali." Ingawa katika tafsiri wameifasiri vilivyo.

20. Na utakapoyaona (yaliyoko) huko utaona neema (zisizo kuwa na mfano) na ufalme mkubwa.

21. Juu yao wana nguo za hariri laini, za kijani kibichi na za hariri nzito. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao atawanyweshwa kinywaji safi kabisa.

22. (Awaambie): "Hakika haya ni malipo yenu; na amali zenu zimekubaliwa."

23. Hakika sisi tumekuteremshia Qurani sehemu sehemu (kidogo kidogo).

24. Basi ngojwa hukumu ya Mola wako wala usimtii miongoni mwao mwenye kufanya, madhambi au mwenye kukufuru.

25. Na likumbuke (litaje) jina la Mola wako asubuhi na jioni;

26. Na usiku msujudie Yeye, na umtukuze usiku, (wakati) mrefu.

27. Kwa hakika watu hawa wanayafadhilisha, (wanayapenda) maisha ya kiduniani na wanaacha nyuma yao (wanaacha kuishughulikia) siku nzito (hiyo ya Akhera inayowangoja).

28. Sisi tumewaumba na tukavitia nguvu viungo vyao. Na tukitaka tutawaleta wengine badala yao walio kama wao.

29. Hakika huu ni ukumbusho; basi anayetaka atashika njia ya kwenda kwa Mola wake.

30. Wala hamuwezi kutaka asipotaka Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye ilimu, Mwenye hikima.

31. Anamuingiza anayemtaka katika rehema yake. Na madhalimu amewawekea tayari adhabu iumizayo barabara.

وَإِذَا رَأَيْتَ نَمَّ رَأَيْتَ نَعِيمًا وَمُلْكًا كَبِيرًا ﴿٢٠﴾

عَلَيْهِمْ نِيَابٌ سُنْدُسٌ خُضْرٌ وَاسْتَبْرَقٌ وَوَحْلَةٌ  
أَسَاوِرٌ مِنْ فِضَّةٍ وَسَقَمَهُمْ رُبُّهُمْ شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢١﴾

إِنَّ هَذَا كَانَ لَكُمْ جَزَاءً وَكَانَ سَعْيَكُمْ مَشْكُورًا ﴿٢٢﴾

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ تَنْزِيلًا ﴿٢٣﴾

فَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تُطِعْ مِنْهُمْ آيْمًا أَوْ  
كُفُورًا ﴿٢٤﴾

وَادْكُرْ اسْمَ رَبِّكَ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٢٥﴾

وَمِنَ اللَّيْلِ فَاسْجُدْ لَهُ وَاسْبِحْهُ لَيْلًا طَوِيلًا ﴿٢٦﴾

إِنَّ هَؤُلَاءِ يُجِبُّونَ الْعَاجِلَةَ وَيَذُرُونَ  
وَرَاءَهُمْ يَوْمًا ثَقِيلًا ﴿٢٧﴾

نَحْنُ خَلَقْنَاهُمْ وَشَدَدْنَا أَسْرَهُمْ، وَإِذَا شِئْنَا

بَدَّلْنَا أَمْثَلَهُمْ تَبْدِيلًا ﴿٢٨﴾

إِنَّ هَذِهِ تَذْكِرَةٌ، فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذَ إِلَى


رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿٢٩﴾

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ

كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٠﴾

يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ وَالظَّالِمِينَ

أَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٣١﴾



Ina Aya 50

## SURATUL MURSALAT

Ina Makara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa (pepo) zinazoletwa kwa upole
2. Na kwa (pepo) zinazovuma kwa kasi
3. Na kwa (pepo) zinazopeperusha (mawingu) mpeperusho (autakao mwenyewe Mwenyezi Mungu)
4. Zikayafarikisha mbalimbali (hayo mawingu)
5. Na naapa kwa (Malaika) wanaopeleka mawaidha (kwa Mitume)
6. Kwa ajili ya kuondosha udhuru au kuhadharisha. (Wasije wakasema kuwa hawakuletewa mawaidha)
7. Hakika haya mnayoahidiwa, bila shaka yatatokea.
8. Wakati nyota zitakapofutwa (nuru zake)
9. Na mbingu zitakapopasuliwa
10. Na milima itakaposagwasagwa
11. Na Mitume watakapokusanywa (katika wakati maalumu huo uliowekwa)
12. Kwa siku gani hiyo wamewekewa muda huo?
13. Siku ya hukumu.
14. Na nini kitakachokujulisha siku ya hukumu (ni nini? Ni siku gani hiyo)?
15. Ole wao, (adhabu itawathubutikia) siku hiyo hawa wanaokadhibisha!
16. Je! hatukuwaangamiza (watu) wa zamani (kabisa)?

وَالْمُرْسَلَاتِ عُرْفًا ۝

فَالْعَصْفِ عَصْفًا ۝

وَاللَّشْرِبِ نَشْرًا ۝

فَالْعُرْفِ عُرْفًا ۝

فَالسَّقِيَةِ ذِكْرًا ۝

عُدْرًا أَوْ نَذْرًا ۝

إِنَّمَا تُوعَدُونَ لَوَاقِعٌ ۝

فَإِذَا النُّجُومُ طُيَسَتْ ۝

وَإِذَا السَّمَاءُ فُرِجَتْ ۝

وَإِذَا الْجِبَالُ سُفِكَتْ ۝

وَإِذَا الرَّسُلُ أُؤْتِنَتْ ۝

لَأَيَّ يَوْمٍ أُحِجَّتْ ۝

لِيَوْمِ الْقَضَى ۝

وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمُ الْقَضَى ۝

وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ۝

أَلَمْ نُهْلِكِ الْأَوَّلِينَ ۝

8. Katika Aya hii waliyoifanya ya 9 wanaona kuwa Mwenyezi Mungu anataja yatakatoyotokea mbinguni kitakapoadia Kiama; wao wanasema: "Nyota muradi wake mashekhe. . "

17. Kisha tukawaandamizia (watu) wengine.
18. Basi hivi ndivyo tutakavyowafanya wakosa (wengine).
19. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
20. Je! Hatukukuumbeni kwa maji yaliyo dhalili? (Manii — mbegu ya uzazi)?
21. Kisha tukayaweka mahali pa utulivu,
22. Mpaka muda maalumu
23. Na tukakadiria (wakati wa kutoka mtoto) Nasi ni wazuri kabisa wa kukadiri.
24. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
25. Je! Sisi hatukuifanya ardhi kuwa yenye kukusanya (viumbe)
26. Vilivyo hai na wafu
27. Na ndani yake tukaweka milima mirefu yenye kuthubutu na tunakunywesheni maji matamu.
28. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
29. (Wataambiwa siku ya Kiama); “Nendeni katika ile (adhabu) mliyokuwa mkiikadhibisha.
30. “Nendeni katika kivuli (cha Moto) chenye mapande matatu ”
31. Hakiwafuniki kivuli (hicho) wala hakiwaepushii mwako wa Moto (wa Jahanamu).
32. Hakika (Moto huo) hutoa macheche yaliyo kama majumba .
33. Kama kwamba ni magamia wa rangi ya manjano.
34. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
35. Hii ni siku ambayo hawatasema (kitu)
36. Wala hawatapewa ruhusa (kutoa udhuru) wakapata kutoa.

ثُمَّ نَتَّبِعُهُمُ الْآخِرِينَ ﴿٢٧﴾  
 كَذَلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِينَ ﴿٢٨﴾  
 وَيَلْ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٩﴾  
 أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِنْ مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٣٠﴾  
 فَجَعَلْنَاهُ فِي قَرَارٍ لَّكِينٍ ﴿٣١﴾  
 إِلَىٰ قَدَرٍ مَّا تَكْفُرُونَ ﴿٣٢﴾  
 فَتَقَدَّرْنَا ۖ فَنِعْمَ الْقَادِرُونَ ﴿٣٣﴾  
 وَيَلْ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٤﴾  
 أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ كِفَاتًا ﴿٣٥﴾  
 أَحْيَاءَ وَآمَاتًا ﴿٣٦﴾  
 وَجَعَلْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ شَاخِصَاتٍ وَأَسْقَيْنَكُم مَّاءً  
 فَرَاتًا ﴿٣٧﴾  
 وَيَلْ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٨﴾  
 إِنَّا نَطِّيقُوا إِلَىٰ مَا كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٣٩﴾  
 إِنَّا نَطِّيقُوا إِلَىٰ ظِلِّ ذِي ثُلُثِ شَعْبٍ ﴿٤٠﴾  
 لَا ظِلِّيلٍ وَلَا يُغْنِي مِنَ اللَّهَبِ ﴿٤١﴾  
 إِنَّهَا تَرْمِي بِشَرِّهَا كَالْقَصْرِ ﴿٤٢﴾  
 كَأَنَّهُ جِلَّتْ صَفْرًا ﴿٤٣﴾  
 وَيَلْ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٤﴾  
 هَذَا يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٤٥﴾  
 وَلَا يُؤْدِنُ لَكُمْ فِعْتًا يَوْمًا ﴿٤٦﴾

25,26. Katika maelezo ya hizi Aya walizozifanya ni za 26-27 wametia chungu ya farumu ili kukataa kupelekwa Nabii Isa mbinguni. Na itikadi hii tumeitia katika marejezo ya Aya ya 54 na ya 55 za Surat Aali-Imran. Na Aya ya 157 Surat annisaa na aya ya 117 ya Suratil Maida.

28-40. Yanatajwa yatakayowapata wabaya, kama katika Suratud Dahr yalivyotajwa yatakayowapata watu wema.

37. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
38. (Waambiwe): "Hii ni siku ya Hukumu, tumekukusanyeni nyinyi na waliotangulia."
39. "Ikiwa mnayo hila (ya kujiepusha na adhabu) ifanyeni juu yangu."
40. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
41. Bila shaka wamchao Mungu watakuwa katika vivuli na mito
42. Na matunda (namna namna) wanayoyapenda.
43. (Waambiwe): "Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda."
44. Namna hivi sisi tunawalipa watendao mema.
45. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
46. Kuleni na mjifurahishe kidogo tu (nyinyi makafiri, hapa duniani). Hakika nyinyi ni maasi, (basi mtapata tu adhabu Akhera).
47. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
48. Na wakiambiwa: "Inameni (kuabudu)," hawainami.
49. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha!
50. Basi simulizi gani baada ya hizi (simulizi za Qurani) wataziamini?

- وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٧﴾  
هَذَا يَوْمُ الْقَضَىٰ ، جَمَعْنَاكُمْ وَالْآكِلِينَ ﴿٣٨﴾  
فَإِنْ كَانَ لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيدُوا ﴿٣٩﴾  
وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٠﴾  
إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي ظِلِّ وَعُيُونٍ ﴿٤١﴾  
وَأَفْوَاكِهِمْ يَتَشَهُونَ ﴿٤٢﴾  
كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾  
إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٤٤﴾  
وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٥﴾  
كُلُوا وَتَمَتَّعُوا قَلِيلًا إِنَّكُمْ مُّجْرِمُونَ ﴿٤٦﴾  
وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٧﴾  
وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ ارْكَعُوا لَا يَرْكَعُونَ ﴿٤٨﴾  
وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾  
فَمَا لَكُمْ حَدِيثًا بَعْدَهُ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٠﴾



Ina Aya 40

SURATUN NABAA

Ina Makkara 2

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Wanaulizana habari gani?
2. Ile habari iliyo kuu (ya kufufuliwa viumbe)
3. Ambayo wanakhitalifiana
4. Nawakome! (Wasikhitalifiane). Hivi karibuni watajua (ukweli wake)
5. Kisha nawakome! Hivi karibuni watajua (ukweli wake).
6. Je! Hatukuifanya ardhi kuwa tandiko
7. Na milima kuwa kama vigingi (vya ardhi)
8. Na tukakuumbeni wanaume na wanawake
9. Na Tukaufanya usingizi wenu kama kufa
10. Na tukaufanya usiku kama guo (mnaofunikwa)
11. Na tukaufanya mchana kama kufufuka.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

عَمَّ يَتَسَاءَلُونَ ۝

عَنِ النَّبَاِ الْعَظِيمِ ۝

الَّذِي هُمْ فِيهِ مُتَّفِقُونَ ۝

كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ۝

كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ۝

أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِطًا ۝

وَالْجِبَالَ أَوْتَادًا ۝

وَعَاقَلَكُمْ أَرْوَاجًا ۝

وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ مُمِيًا ۝

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ۝

وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ رِجَافًا ۝

2. Habari kubwa ambayo makafiri walikuwa wakiulizana wenyewe kwa wenyewe, ni habari ya Utume wa Bwana wetu Muhammad (s.a.w.). Walikuwa wakiulizana: Ni kweli huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu? Na hili analodai kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu, na kuwa kuna siku ya Kiama, ni hakika mambo haya?

4. Tamko hili "Kallaa" limekuja mara kwa mara katika Qurani. Na mara huja kwa maana ya "Kukanya" (kukataza), na mara nyingine huja kwa maana ya "kukana" (kukanusha), na mara nyingine huja kwa maana ya "Kukokoteza" (kuthibitisha au kuhakikisha). Na kila mahali hufasiriwa kwa ifaavyo.

5. Mwenyezi Mungu anawaambia hapa kuwa wakome, wawache kudhani mambo ya batili Wakiwa hawajajua hata sasa kwamba Muhammad ni Mtume, na Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu, na kuwa kuna Siku ya Mwisho ya kila mtu kulipwa kwa alilolitenda, basi hapo, yaani Siku ya Kiama, itawafunukia kweli, na watajua kwamba aliyokuwa akiwaambia Mtume ni ya kweli.

6. Tangu Aya hii mpaka Aya 16 Mwenyezi Mungu anawaonesha waja Wake neema nyingi alizowaneemesha, ili wafahamu kwamba, Mwenye kuneemesha neema kama hizi katika Ulimwengu, hawawachi waja Wake katika upotevu pasi na kuwaletea mtu wa kuwaongoa njia njema ya kuwafikisha katika neema za Dunia na Akhera, na kwamba Mwenye kufanya yote haya hapana jengine liwezalo kumshinda. Na maana ya "Tandiko" hapa ni mahali pa kumfaa mtu kufanya alitakalo katika maisha yake. Si mapendeleo yake kuwa Ardhi imekaa kama Tandiko la bitanda. (Taz. Sawi, katika Sura ya *Al-Ghashiyah*.)